# Halo kutoka Madagascar!

Habari, sisi ni Margo na Paolo.

Tunasafiri kuzunguka ulimwengu kujifunza kuhusu watoto wa Mungu. Jiunge nasi tunapozuru Madagascar!





**Madagaska** ni kisiwa kilichopo pwani ya mashariki ya Afrika. Kina mimea mingi na wanyama wengi ambao hawapatikani sehemu yo yote duniani—komba wa bukini mwenye mkia wa duara!



Wavulana hawa wanasaidia kubeba majagi ya maji kwa ajili ya familia zao Je, unaisaidiaje familia yako?





Kanisa ni dogo katika Madagaska, lakini linakua! Kwa sasa kuna kata 14 na matawi 26 huko.



Aina zaidi ya vinyonga huishi nchini Madagaska kuliko mahali pengine popote ulimwenguni!



Miti hii mikubwa ya mibuyu inaweza kuhifadhi maji mengi kwenye mashina yake hadi lita 120,000!



Watu wengi nchini Madagaska hula wali mara mbili au tatu kwa siku, wakati mwingine na mboga, maharagwe, au nyama.

Namana!



Neno “rafiki” Kimalagalasi ni *namana* Ikiwa ungekutana na rafiki mpya huko Madagaska, ungewaambia nini?

VIELELEZO NA KATIE MCDEE

## Kutana na baadhi ya marafiki zetu kutoka Madagaska!



Ninajua kwamba Yesu Kristo ni Mwokozi wetu.

**Nathan, miaka 7, Jimbo la Antananarivo, Madagaska**



Russell M. Nelson ni nabii wa Mungu.

**Nomena, miaka 6, Jimbo la Antananarivo, Madagaska**

**Je, wewe unatokea Madagaska? Tuandikie Tungependa kusikia kutoka kwako.**



Asante kwa kutalii Madagascar pamoja nasi. Tutaonana wakati mwingine!